

MKATABA WA KUPANGISHA ENEO LA BIASHARA

(LEASE AGREEMENT)

Mkataba huu umefanyika leo tarehe¹².....Mwezi.....².....2024

Kati ya

WALTER CAMILUS LEKULE ambayo hapa kwenye mkataba huu anatambulika kama
"MPANGISHAJI".

NA

LEVITIQUE GENERAL BUSINESS AND TRADING LIMITED yenye nambari ya
usajili 157-238-043 ambayo hapa kwenye mkataba huu inajulikana kama "MPANGAJI"

MPANGISHAJI NA MPANGAJI KWA PAMOJA WAMEKUBALIANA

KWAMBA:-

1. KODI/MALIPO NA MUDA WA MKATABA

- a) Mwenye eneo amempangisha Mpangaji chumba cha ofisi kilichopo **MBEZI BEACH "B" ST. K AWE, KINONDONI, DSM** kwa kipindi cha miezi sita (6) kwa malipo ya 100,000 TZS (LAKI MOJA Tu) kwa kila mwezi, ambazo zitalipwa zote kwa pamoja.

2. MAKUBALIANO MENGINE NI KWAMBA:

- a) Mpangaji atatumia Fremu hiyo kwa ajili ya biashara tu.
- b) Mpangaji ataheshimu sheria zote na taratibu halali zinazokubalika na jamii ili kudumisha usalama watu na mali zao.
- c) Mpangaji ataweka Fremu hiyo katika hali ya usafi wa kuridhisha nje na ndani ya Fremu ikiwa ni pamoja na utunzaji wa kuta, milango, madirisha, nyaya na vifaa vya umeme ambavyo ni **MALI YA TANESCO** vilivyomo kwenye nyumba.
- d) Mpangaji haruhusiwi kumpangisha au kubadilishana upangaji na mtu mwingine (kupasiana pango au ku sub-lease/let) Fremu aliyopangishwa, pia asiye akafanya

matengenezo yoyote ya kiujenzi katika nyumba hiyo bila ya kushauriana na kupata kibali kutoka kwa **Mwenye Nyumba**.

- e) **Mpangaji** atamruhusu **Mwenye Nyumba** au/na **Maofisa Wakaguzi wa Luku** kutoka **TanESCO** kuingia muda na wakati unaofaa (official hours) kuona na kufanya matengenezo yatakayohitajika baada ya kupeana taarifa na **Mpangaji Au Mwakilishi Wake** ilimradi matengenezo hayo hayatachukua muda mrefu au kusababisha uhamishaji nje wa vifaa ndani ya nyumba.
- f) **Mpangaji** atamruhusu **Mwenye Nyumba** kufanya matengenezo yanayoweza kuhitajika kwenye Fremu ilimradi hayatamletea **Mpangaji** bugudha au kusababisha kuhamisha vifaa vyake vyote ndani ya Fremu. Hili litafanyika baada AU kwa kadiri watakavyo kubaliana mpangaji na Mwenye nyumba.
- g) Mpangaji atalipia umeme (LUKU) na Maji kulingana na matumizi yake kwa muda unaohitajika.

3. PIA PANDE ZOTE ZIMEKUBALIANA KWAMBA:

- a) **Mwenye nyumba** atalipia kodi ya kiwanja (Land fee), kodi ya Majengo (Property Tax) na zinginezo kwa mujibu wa sheria za Halmashauri ya mji.
- b) Endapo **Mpangaji** atanuia kuendelea kupanga Fremu hii kwa kipindi kingine baada ya kipindi cha mkataba huu kumalizika, na ikiwa nia yake ipo, atampa Mwenye nyumba taarifa kwa maandishi si chini ya siku 30 (Mwezi mmoja) kabla ya kumalizika kwa kipindi kilicho kubaliwa katika mkataba huu na iwapo hakuna ukiukaji wa makubaliano yoyote yaliyo katika mkataba huu.
- c) Endapo kutatokea dharura kwa upande wa mwenye nyumba kuhitaji Fremu hiyo kabla ya muda wa mkataba huu kumalizika, Mwenye nyumba atampa Mpangaji taarifa ya **Miezi 2 (Miwili)** kutoka kwenye Fremu hiyo. Vilevile Mpangaji atampa Mwenye nyumba taarifa isiyopungua **Miezi 2** endapo ataamua kuachia nyumba hiyo (kutoka/kuacha pango)
- d) Mpangaji atahakikisha kuwa haachi **"Outstanding Bills"** zake zozote endapo atahitajika kutokuendelea na mkataba.

e) Ifahamike wazi kuwa iwapo Mpangaji atalipa kodi waliyokubaliana katika mkataba huu, na kulipa bills zake inavyopaswa, atakaa kwenye hii nyumba bila kusumbuliwa na mtu yoyote.

HIVYO BASI, pande zote mbili zimekubaliana kama inavyoelezwa hapo juu kwenye mkataba huu na wamethibitisha kwa sahihi zao hapa chini;-

MPANGISHAJI WA OFISI

Jina: WALTER CAMILUS LEKULE

Saini: *W. Lekule*

Cheo: *Mfanyabi* 12-2-2024

JINA LA MPANGAJI WA OFISI

LEVITIQUE GENERAL BUSINESS AND TRADING LIMITED

Jina la Mkurugenzi Mtendaji: ~~JAMES CASTORY KIWALE~~ MICHAEL MICAMIAS ZENG

Saini: *[Signature]*

Cheo: *M.D.*
12/2/24

MAKUBALIANO YAMEFANYIKA MBELE YA:

JINA: *James Castory Kiwale*

CHEO: *D. S. Jay*

SAINI: *[Signature]*

TAREHE: 12/02/2024



STAMP DUTY
TSh. 18,000/- collected
Receipt No. 9984114984843 Date 13/02/2024
Regional - Manisa - Tanga Tax Region